

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**



**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA AROBAINI**

**08 JUNI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

**KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 08 JUNI, 2022**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**353. MHESHIMIWA SEIF SAID GULAMALI  
(MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono Wananchi wa Jimbo la Manonga kwa kuwasidia kujenga madarasa mawili katika kila shule.

**354. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI  
(CHEMBA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Maboma ya Zahanati za Kinkima, Rofat, Tumbakose, Songolo na Sori Wilayani Chemba.

**355. MHESHIMIWA DAIMU IDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Kituo cha Afya Mtina kitaboreshwa ili kutoa huduma ya upasuaji pamoja na kupeleka Vifaa Tiba katika Kituo cha Afya Mchoteka.



**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**356. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Bodi ya mitaji kwa wahitimu wa elimu ya juu kama ilivyo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**357. MHESHIMIWA SHABAN OMARI SHEKILINDI  
(LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Lushoto.

**358. MHESHIMIWA ASIA ABDULKARIM  
HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**359. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL  
KUNAMBI (MLIMBA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya Wananchi na TAWA katika Bonde la Mto Kilombero.

**360. MHESHIMIWA JEREMIAH MRIMI AMSABI (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itaweka alama za mipaka katika Hifadhi ya Serengeti na Pori la Akiba la Ikorongo ili kumaliza migogoro na Vijiji jirani.



**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**361. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHWALE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaongeza geti jingine ndani ya Jimbo la Momba kutokana na geti la Tunduma kuzidiwa katika kutoa huduma.

**WIZARA YA KILIMO:**

**362. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED  
ABDALLAH (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Kilimo katika eneo la Ngongo Mkoani Lindi ambapo tayari hekari 120 zimetengwa kwa ajili hiyo.



**DODOMA  
08 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**